**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE ZA SEKONDARI ZA SERIKALI TANZANIA

**MEI, 2025**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS – TAMISEMI**

**Namba za simu;**
**Mkuu wa Shule 0786617866**
**Makamu M/Shule 0622356248**

**Shule ya Sekondari LUPIRO**
**S.L.P.288**
**Ulanga**
**Morogoro**
**Tarehe .21/04/2025**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ………….**
**……………………………………………..**
**S.L.P ……………………………………..**
**…………………………………………….**

Yah**: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI LUPIRO HALMASHAURI YA ULANGA MKOA MOROGORO MWAKA 2025**

**1.**Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato chaTano katika Shule hii mwaka 2025 na atasoma tahasusi ya **PCB/PCM**

**Shule ya Sekondari LUPIRO inapatikana katika walaya ya Ulanga umbali wa Kilometa 2 toka kituo cha mabasi lupiro. Usafiri wa basi kutoka mjini IFAKARA unapatikana katika kituo cha mabasi KIBAONI AU unaweza kupanda gari za moja kwa moja toka MOROGORO au DAR ES SALAAM zinazoelekea MALINYI AU MAHENGE/ULANGA na shuka katika kituo cha mabasi LUPIRO.**

**Muhula wa Masomo unaanza tarehe 08/07/2025, hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe 07/07/2025 Mwisho wa kuripoti ni tarehe 31/07/2025,**

**2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-**

**2.1 SARE ZA SHULE**

i. Sketi mbili light blue
ii. Shati mbili za mikono mirefu zenye nembo ya shule zinapatikana shuleni
iii. Kwa waislam nusu kanzu na Hijab (kijuba) zenye nembo, zinapatikana shuleni
iv. Sare ya Michezo ni track suti (moja) light blue, jezi (moja) ya nyekundu na pea ya raba rangi yeyote.
v. Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi.
vi. Soksi jozi mbili nyeupe
vii. Sweta (moja);linapatikana shuleni lenye nembo
viii. Nguo za kushindia (*shambadress*) gauni mbili za kijivu
ix. Tai mbili za light blue
x. T/sheti (T-shirt) darkblue (moja) yenye nembo ya shule inapatikana hapa shuleni.

**Gharama mavazi yaliyopo shuleni kama utahitaji kuyapata hapa shuleni;**-

a) Sketi shs. 30,000/= @ moja
b) Shati shs. 13,000/= @ moja
c) Tai shs. 5,000/=@moja
d) tracksuit shs. 25,000/= @ moja
e) t-sheti shs. 15,000/= @ moja
f) jezi shs. 12,000/=@ moja
g) Shamba dress shs. 30,000/= @ moja
h) Nusu kanzu na hijabu yake shs 40,000/= @ moja
i) Sweta moja yenye nembo ya shule shs 20,000/= @ moja

**2.3 MAHITAJI MENGINE MUHIMU AMBAYO MWANAFUNZI ANAPASWA KUJA NAYO SHULENI: -**

i. Madaftari **11** counter book quire 3 au four
ii. **Ream (A4)** ya Karatasi Mbili (2) kwa mwaka;
iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika kama, chands book kwa fizikia, biological science kwa biolojia,pure 1& 2, tlunter kwa hesabu.
iv. Dissecting Kit kwa wanafunzi wanaosoma Biology;

v. Scientific Calculator;
vi. Godoro ft 2.5 kwa ft 6;
vii. Sanduku (tranka)
viii. Mashuka Jozi 2 pink, blanket 1 rangi yeyote, foronya ya godoro 1, chandarua 1 *rangi ya pink*
ix. Nguo za ndani za kutosha;
x. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe);
xi. Ndoo kubwa 1 na ndogo 1 zenye mifuniko;
xii. PCM waje pia na Kwanja 1, jembe 1, squeezer 1, hardbloom 1 na soft bloom 1

PCB waje pia na Kwanja 1, jembe 1, Mopper 1, hardbloom 1 na soft bloom 1

### 2.4 MICHANGO MBALIMBALI

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| **1.** | **Mchango wa uendeshaji wa shule** | **65,000/=** |
| **2.** | **Tahadhari** | **5,000/=** |
| **3.** | **Nembo** | **5,000/=** |
| **4.** | **Kitambulisho** | **5,000/=** |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

Malipo Yafanyike Kupitia **NMB A/C: 21906600083**
**JINA: LUPIRO SECONDARY SCHOOL**

## SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye

jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 SHERIA NA KANUNI ZA SHULE

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;

ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;

iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);

iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;

v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;

vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;

vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;

viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;

ix. Kutunza mali za shule;

x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na

xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**
- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**
- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

### 3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:

i. Wizi;

ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;

iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;

iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba; Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiii. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xiv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xv. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvi. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu;
xvii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**Viambatisho na Fomu Muhimu**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO**

**WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule 0786617866**
- **Makamu Mkuu wa Shule 0784916941**
- **Mwandamizi Taaluma 0625135028**
- **Malezi 0685991995**

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

**Saini ya Mkuu wa Shule ………………………………………**

**Jina la Mkuu wa Shule ANNETH M. CHENGULA**

**Mhuri wa Mkuu wa Shule ………………………………..**

PRESIDENT`SOFFECE
REGIONALADMINISTRATION AND LOCALGOVERNMENT

SHULEYA SEKONDARILUPIRO,
S.L.P 288,
MAHENGE/ULANGA.
________________________

REQUESTFOR MEDICALEXAMINATION

Please examine _______________________________________as to his/her physical and mental
Fitness for admission as a form FIVE at Lupiro Secondary School for the Academic year 2025/2026.

YoursSincerely.

…………..……………………..

ANNETH M. CHENGULA
THE HEADMISTRESS

The Headmistres, I have examined __________________________________as shown below and consider that she is physically and mentally fit/unfit for admission to pursue a full-time Secondary School education.

1. Vision with/without glasses.
   Right______________________________________
   Left_________________________________________
2. Bloodpressure_____________________________________________________
   Humoring______________________________________________
3. Hearing__________________________________________________________
4. (a)Urine Albumen______________________________________________
   (b)Sugar_____________________________________________________
5. (a) Venereal disease______________________________________________
   (b) Bilharzias_________________________________
6. Pregnancy___________________________________
7. Neurosis_____________________________________________
8. Is there any abnormality of:-
   (a)The heart_______________________ (b)Lungs________________________
   (c)The spleen________________________
9. Are there any serious e.g.leprosy,diabetes,etc
   _________________________________________________________________

Date__________________________________
Station_______________________________
Signature of medical officer________________________
Designation____________________

KIAMBATISHO “C”

Ndugu wa karibu: Hakikisha unaandika majina na anwani zao. Hii
Inasaidia shule kutoa taarifa endapo tatizo linatokea. Hatutaki majina ya ndugu wa bandia.

1. (a)Jina……………………………..…….(b)Uhusiano…………………….……
   (c)Anuani………………………………………………………………………
   (d)Kata………………………………. (e)Mtaa……………………...………
   (f)Namba ya simu …………………………..

2. (a)Jina……………………………..…….(b)Uhusiano…………………….……
   (c)Anuani………………………………………………………………………
   (d)Kata………………………………. (e)Mtaa……………………...……
   (f)Namba ya simu …………………………..

3. (a)Jina……………………………..…….(b)Uhusiano…………………….……
   (c)Anuani………………………………………………………………………
   (d)Kata………………………………. (e)Mtaa……………………...………
   (f)Namba ya simu …………………………..

4. (a)Jina……………………………..…….(b)Uhusiano…………………….……
   (c)Anuani………………………………………………………………………
   (d)Kata………………………………. (e)Mtaa……………………...………
   (f)Namba ya simu …………………………..

Sahihiyamzazi…………………………………………..
Tarehe…………………………………………………..

AHADIYA KUTELEKEZA WAJIBU

Mimi……………………………………………………nakubali nafasi niliyopata katika Shule ya Sekondari ya Lupiro kuendelea na masomo. Nafahamu kuwa nimegharamiwa na Taifa linalothamini kazi na juhudi.

Naahidi mbele ya mzazi/mlezi wangu kuwa nitajitahidi kwa upeo nauwezo wangu Kuwa mwanafunzi mwema.

Ninaahidi kutoshiriki katika mambo yatakayosababisha mwanafunzi kuachishwa shule.

Naahidi kuwa nitashirikiana na walimu/malezi pamoja na wanafunzi wezangu katika Kila jambo lenye manufaa kwa shule yangu na Taifa kwa ujumla.

……………..

Sahihi ya mwanafunzi

Mimi…………………………………………………………mzazi/mlezi wa………………………………..………………...Nimesoma maelezo yote na kuelewa. Naahidi kwamba nitampatia mahitaji yote kama ilivyoagizwa katika barua. Ripoti na barua zote zinazohusu motto wangu ziletwe

Kwangu kwa anuani hiyo hapo chini:-

S.L.P……………………………………………..

……………………………………………………

……………………………………………………

Jina la mzazi…………………………………….…Saini …………………

Namba ya simu……..…………

KIAMBATANISHO “D”

FOMU YA MKATABA

A.KATI YA MWANAFUNZI NA SHULE.

1.Jina kamili kama alivyoandikishwa kwenye mtihani……………………………………

2.Tarehe ya kuzaliwa…………………………………………………………………

3.Mahali alipozaliwa…………………………………………………………………

4.Dini…………………………………………………………………………………

5.Shule alipomaliza elimu ya msingi …………………………..

Wilaya………………….Mkoa………………………. Mwaka aliomaliza…………

6.Shule alipomaliza elimu ya sekondari (kidatochanne) …………………………..

Wilaya……………………….....Mkoa………………………………Mwaka……

Mimi…………………………………….Ninaahidi kutoshiriki mgomo, fujo na makosa ya jinai kama yaliyoainishwa katika sheria zashule na nchi kwa ujumla.

Sahihi…………………………………………………Tarehe…………………

B.KATIYA MZAZINA SHULE.

Mimi…………………………………………………….…………Mzazi/Mlezi wa……………………………………..

Ninakiri na kukubaliana na sheria za shule kama ambavyo zimeainishwa kuwa Mwanangu hatashiriki mgomo,fujo na makosa mengine ya jinai.

Aidha, nitakubaliana na hatua za kisheria atakazochukuliwa mwanangu……………………………………………….endapo atakiuka taratibu za hule.

Sahihi…………………………………………………Tarehe…………………… ………………...